



Kumb Na.: HWB/A.20/76/218

Tarehe: 13 Julai, 2024

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri` ya Wilaya ya Bagamoyo amepokea kibali cha Ajira mpya kutoka kwa Katibu Mkuu OR-Utumishi chenye **Kumb. Na. FA.97/200/01/09** cha tarehe **25/06/2024**. Hivyo anapenda kuwatangazia Watanzania wote wenye sifa kutuma maombi kwa kada mbili (02) kama zilivyoainishwa kwa kuzingatia sifa tajwa.

### 1.0 MWANDISHI MWENDESHA OFISI DARAJA LA DARAJA II – NAFASI - 5

#### 1.1 KAZI NA MAJUKUMU YA MWANDISHI MWENDESHA OFISI.

- i. Kuchapa barua, taarifa, nyaraka za kawaida na za siri.
- ii. Kupokea wageni na kuwasaili shida zao na kuwaelekeza wanapoweza kusaidiwa.
- iii. Kutunza taarifa za kumbukumbu ya matukio, miadi, tarehe za vikao, safari za Mkuu wake na ratiba za kazi zingine.
- iv. Kutafuta majalada na nyaraka zinazohitajika katika utekelezaji wa majukumu ya kazi.
- v. Kupokea majalada na kusambaza kwa maofisa walio katika Idara/Kitengo/Sehemu husika.
- vi. Kukusanya, kutunza na kuyarejesha majalada na nyaraka sehemu zinazohusika.
- vii. Kupanga dondo na kufanya maandalizi ya vikao mbalimbali.
- viii. Kuandaa orodha ya mahitaji ya vifaa vya Ofisi na
- ix. Kufanya kazi zingine atakazopangiwa na Mkuu wake wa kazi.

#### 1.1.1 SIFA ZA MWOMBAJI.

Kuajiriwa mwenye Elimu ya Kidato cha Nne (Form IV) au Kidato cha Sita (Form VI) aliyehitimu mafunzo ya Stashahada/Diploma (**NTA Level 6**) ya Uhazili na awe amefaulu somo la Hatimkato ya Kiswahili na Kiingereza maneno 100 kwa dakika moja na kupata Progamu ya Kompyuta za Ofisi kama vile Word, Excel, Powerpoint, Internet, E-mail na Publisher kutoka chuo chochote kinachotambuliwa na Serikali.

#### 1.1.2 NGAZI YA MSHAHARA.

Kwa kuzingatia viwango vya mishahara ya Serikali **TGSC**

## **2.0. MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU DARAJA II (Records Management Assistant II) NAFASI - 5**

### **2.1 KAZI NA MAJUKUMU YA MSAIDIZI WA KUMBUKUMBU II.**

- i. Kutafuta Kumbukumbu/Nyaraka/Mafaili yanayohitajika na wasomaji.
- ii. Kudhibiti upokeaji, uandikishaji wa Kumbukumbu/Nyaraka.
- iii. Kuchambua, kuorodhesha na kupanga kumbukumbu/Nyaraka katika makundi kulingana na somo husika (Classification and Boxing) kwa ajili ya matumizi ya Ofisi.
- iv. Kuweka/kupanga kumbukumbu/nyaraka katika reki (File Racks/Cabinets) katika masijala/vyumba vya kuhifadhi kumbukumbu/nyaraka.
- v. Kuweka kumbukumbu (barua, nyaraka nk.) katika mafaili.
- vi. Kushughulikia maombi ya Kumbukumbu/Nyaraka kutoka Taasisi za Serikali.
- vii. Kutekeleza kazi zozote atakazokuwa amepangiwa na Msimamizi wake wa kazi.

#### **2.1.1 SIFA ZA MWOMBAJI.**

Awe na Elimu ya Kidato cha nne (Form IV) au cha Sita (Form VI) aliyehitimu mafunzo ya Stashahada/Diploma (**NTA Level 6**) katika Fani ya Masijala kutoka vyuo vinavyotambuliwa na Serikali, wenyewe ujuzi wa Kompyuta.

#### **2.1.2 NGAZI YA MSHAHARA.**

Kwa kuzingatia Ngazi za Mishahara ya Serikali – **TGS C**

#### **MASHARTI YA UJUMLA KWA WAOMBAJI**

- i. Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania wenyewe umri wa miaka **18** na usiozidi miaka **45** isipokuwa kwa wale tu walioko kazini Serikalini.
- ii. **Waombaji wenyewe ulemavu wanahamasishwa kutuma maombi na wanapaswa kuainisha kwenye mfumo wa kuombea ajira aina ya Ulemavu walionao kwa ajili ya taarifa kwa Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma.**
- iii. Waombaji waambatanishe maelezo binafsi yaliyojitosheleza **Carriculum Vitae (CV)** yenye Anuani inayotumika, namba za simu zinazopatikana na **Anuani ya barua pepe (E-mail adress)** pamoja na majina ya wadhamini (**Referees**) watatu wa kuaminika.
- iv. “Provisional “/Testimonials”/ “Statement of results” na hati za matokeo za kidato cha Nne na Sita (Form IV and Form VI results slip) **HAVITAKUBALIWA**.
- v. Waombaji wote waambatanishe cheti cha kuzaliwa kilichothibitishwa na Mwanasheria/Wakili.
- vi. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali cha Katibu Mkuu Kiongozi.

- vii. Waombaji ambao tayari ni Watumishi wa Umma na wamejipatia sifa za kuingia katika kada tofauti na walizonazo, wapitishe barua zao za maombi ya nafasi za kazi kwa waajiri wao na waajiri wao wajiridhishe ipasavyo.
- viii. Waombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma, wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka **Na. CAC.45/257/01/D/140** wa tarehe **30 Novemba, 2010**.
- ix. Maombi yote yaambatane na vyeti vya taaluma vilivyothibitishwa na Mwanasheria/Wakili ambavyo ni vyeti vya Kidato cha Nne, kidato cha Sita kwa wale waliofikia kiwango hicho na vyeti vya kuhitimu mafunzo mbalimbali kwa kuzingatia sifa za kazi husika.  
**Postgraduate/Degree/Advanced Diploma/Dilpoma/Certificates, - Cheti cha mtihani wa Kidato cha IV na VI, - Computer Certificate, - Vyeti vya Kitaaluma (Professional Certificate from Respective Boards).**
- x. Waombaji walisoma nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vimethibitishwa na Mamlaka husika (**TCU, NECTA na NACTE**).
- xi. Uwasilishaji wa Taarifa na Sifa za kughushi, wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- xii. Barua ya maombi iandikwe kwa Kiswahili au Kiingereza.
- xiii. Mwisho wa kupokea barua za maombi ni tarehe **26 Julai, 2024**
- xiv. **MUHIMU:** Kumbuka kuambatanisha barua yako ya maombi ya kazi iliyosainiwa pamoja na vyeti vya elimu, aidha anuani ya barua hiyo ielekezwe kwa:

**Mkurugenzi Mtendaji,**

**Halmashauri ya Wilaya ya Bagamoyo,**

**S.L.P 59**

**BAGAMOYO**

- xv. Maombi yote ya kazi yatumwe kwenye mfumo wa kielektroniki wa ajira (Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatayo; <https://portal.ajira.go.tz> (Anuani hii pia inapatikana kwenye Tovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kuingia sehemu ilyoandikwa "**Recruitment Portal**"
- xvi. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulio ainishwa katika tangazo hili **HAYATAFIKIRIWA.**

**Limetolewa na;**

Shauri Selenda

**MKURUGENZI MTENDAJI**

**HALMASHAURI YA WILAYA**

**BAGAMOYO.**

